



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 22 Mei, 2021.

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. **TAARIFA YA SPIKA:**

II. **MASWALI:**

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

84. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando)
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais,
Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Pamoja na juhudi kubwa za kuimarisha huduma za afya katika Kituo cha Afya Ukunjwi, ambapo hivi sasa huduma za uzalishaji zinapatikana na kuwarahisishia wakaazi wa vijiji vya jirani kupata huduma hizo kwa ukaribu zaidi, licha ya kuwepo kwa changamoto ya madaktari na majengo inayorudisha nyuma huduma za afya katika kituo hiki.

- (a) Je, Serikali imepanga kuchukua hatua gani za haraka kukabiliana na changamoto ya madaktari katika kituo hiki ambacho kina daktari mmoja tu kwa huduma zote zinazotolewa.
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga jengo jipya ambalo litakidhi mahitaji ya huduma za afya katika kituo hiki.

- (c) Je, Serikali haioni kwamba kuendelea kuwepo kwa changamoto hizi ni kuhatarisha afya na maisha ya wakaazi wa Ukunjwi na vitongoji vyake.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

88. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Je, Serikali ina mpango gani juu ya kugawa bendera ya Zanzibar kwenye skuli, ukizingatia kuna skuli ambazo uchumi wao ni mdogo na viongozi wa skuli hizo wanalamika kuwa hawana bendera.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

110. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa barabara ya Fuoni Jitimai inasababisha ajali nyingi na kupelekea wananchi kupata ulemavu wa viungo na wengine hufariki.

Je, ni lini Wakala wa Barabara ataiwekea matuta barabara hiyo

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

81. MHESHIMIWA MOH'D MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweka utaratibu mzuri wa kusimamia na kudhibiti bei za bidhaa muhimu zinatumwa na wananchi wetu.

- (a) Je, kwa sasa bei za bidhaa/vyakula hivyo ni kiasi gani.
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwashughulikia wale wote wanaokwenda kinyume na bei hizo.
- (c) Je, ni vigezo gani ambavyo Serikali hutumia katika kupanga bei za bidhaa hizo.

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

8. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Katika azma ya kukuza uchumi wa Zanzibar hasa Uchumi wa Buluu, Serikali ina mpango wa kununua boti 4 kubwa za uvuvi wa Bahari Kuu.

- (a) Je, Serikali imefanya tathmini ya kutosha kuhusu faida inayoweza kupatikana kwa kuchukua mfano wa boti ya awali ya Mkombozi II iliyo chini ya Kampuni ya ZAFICO.
- (b) Ni kiasi gani cha gharama zilizotumiwa na Serikali na kiwango gani cha faida kimepatikana tokea kuwasili kwa boti ya uvuvi ya MKOMBOZI II.
- (c) Je ni muda gani sasa tokea kuwasili na kuanza kazi kwa meli ya uvuvi ya MKOMBOZI II.

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

46. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale.

Kumekuwa na utaratibu wa wafanyakazi wa sekta ya utalii kutembelea na kuzikagua hoteli ili kujua idadi ya wageni katika hoteli hizo, jambo hilo linasababisha kero kwenye hoteli na wageni wao. Kwa kuwa teknolojia ya mawasiliano imeimarishwa katika maisha ya hivi karibuni.

- (a) Kwanini Serikali haitafuti njia bora na ya uhakika ya kuwatambua wageni wote wanaoingia na kulala katika hoteli zote bila ya kwenda kufanya msako huo.
- (b) Je, ni Mkoa gani wa Zanzibar uliopokea watalii wengi katika kipindi cha Januari/Machi, 2021.

Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

129. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikijitahidi kutoa huduma za afya kwa wananchi wote ingawaje bado kuna usumbufu wa kutopata dawa hasa kwa wagonjwa wanaolazwa katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja. Wagonjwa hao huambiwa wakanunue dawa hizo kwenye maduka ya nje, jambo ambalo husababisha usumbufu mkubwa kwa wagonjwa na jamaa zao.

- (a) Je, Serikali haioni kwamba ni vyema kuanzisha duka la dawa ndani ya eneo la Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja ili kuwapunguzia usumbufu wagonjwa na jamaa zao.
- (b) Ni sababu zipi zinazopelekea mgonjwa kutakiwa kununua dawa nyakati za usiku wakati jamaa zake wameshaondoka.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2021/2022.

Zanzibar,
22 Mei, 2021.

(Raya Issa Msellel)
KATIBU WA BARAZA